JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFIS YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

MKOA WA SONGWE
MTIHANI WA UTIMILIFU KIDATO CHA NNE - 2018
KISWAHILI

MUDA: SAA 3:00

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A,B,C,D na E zenye jumla ya maswali kumi na tano (15)
2. Jibu maswali yote katika sehemu A,B,na D na swali moja (1) kutoka sehem C na maswali matatu (03) kutoka sehemu E. Swali la 15 ni la lazima.
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyo ruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika namba yako ya mtihani katika ukurasa wa kujibibia.

SEHEMU S (Alama 10)

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kasha jibu maswali.

"Zakaria , unamuona Yule kijana anayepita yulee..... ni mwanafunzi wa shule ya sekondari Peramiho. Yeyeni mwingi wa tabia chafu, anajihusisha sana na vitendo vya ngono. Hata hivyo , cha ajabu bado anadunda" Michael alimweleza Zakaria na huku akimnyooshea kidole kijana aliyekuwa akipita.

"Huwezi kumtambua mtu mwenye Ukimwi kwa kumwangalia tu. Mtu mwenye siha nzuri mnene na mtanashati anaweza kuwa na vizusi vya Ukimwi, na mwingine mwenye kuonekana dhaifu na afya isiyoridhisha akawa hana virusi vya Ukimwi. Hivyo umbile au muonekano wa nje wa mtu hauwezi kukuhakikishia kuwa mtu huyo hana virusi vya Ukimwi, wala kukuhakikishia wewe usalama wako dhidi ya maambukizo ya virusi endapo utakuwa na mahusiano naye ya kimapenzi yasiyo salama.

Kumbuka kwamba mtu anaweza kuwa na virusi vya Ukimwi kwa miaka mingi sana bila kuonesha dalili hata moja ya kuwa na maambukizo ya virusi hivyo, achilia mbali dalili za kuwa ana Ukimwi. Hebu fikiria katika kipindi hicho anaweza kuwa ameambukiza wangapi endapo atakuwa na mahusiano ya kimapenzi yasiyo salama, hasa kwa mtu kama huyo kijana unayesema ni mwingi; alijibu: Njia pekee ya kumtambua kama mtu ana virusi vya Ukimwi au la ni kupima. Kwa maneno mengine, njia pekee ya kujihakikishia usalama na kuepukana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi ni ile ya kutoona soo, kuambizana ukweli juu ya kupima damu.

Baada ya kupima, ni kwani kuhakikisha kuwa mnazingatia ushauri mnaopewa, kwani mtu anapopimwa anapewa ushauri nasaha wa namna ya kuishi salama. Baadhi ya vijana wanasikika wakisema eti wana mpenzi mmoja tu, naye ni mwaminifu, hivo hawawezi kuambukizana virusi vya Ukimwi. Hakika huko ni kujipotosha na kujitafutia maangamizi kwani uaminifu huo hauthibitiki bali ni wa kufikirika tu. Wangapi wanavunja uaminifu au watumie kondomu. Vijana husema kuwa ni vema wasione soo wasubiri wawe waaminifu au watumie kondomu. Vijana husema kuwa wataweza wapi kupima?. Eti leo uende ukapime na Mwanaidi , kesho na Salome, kesho kutwa na Mwajuma. Tahadhari kubwa ni lazima wawe nayo katika kujilinda , kujikinga na kujiepusha na vitendo vya ngono.

Ikumbukwe kuwa vijana ni Taifa la kesho, ndiyo nguvu kazi ya jamii inayotegemewa. Bila vijana, kesho hapatakuwa na Taifa. Rais wa kesho atatokana na vijana, Daktari wa kesho yu miongoni mwao, vilevile mwalimu, mhandisi, kasisi, shekhe, mwanasayansi, karani na wengine wote watatokana na kizazi kipya. Kesho inategemea vijana waliopo leo. Kutokana na hilo ni lazima sasa vijana watambue nafasi yao, wajibu wao na majukumu yao kisha wabadili tabia na mienendo isiyofaa. Kijana huko shuleni bado unahangaika nini? Kumbuka mshika mawili.....jamani msione soo!

MASWALI (Alama 05)

i. Andika kichwa cha habari uliyosoma, kisichozidi maneno matano.....
ii. Ka nini huwezi kumtambua mtu mwenye virusi vya Ukimwi kwa kumwangalia tu?
iii. Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari kama yalivyotumika kwenye habari uliyosoma.
iv. Faida za kupima virusi vya Ukimwi ni.....
v. Unafikiri kuwa na mpenzi mmoja ni kinga tosha ya maambukizo ya Ukimwi? Kwa nini?
vi. Ni njia ipi kuu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Ukimwi?
vii. Njia bora ipi kwa vijana ya kujikinga na Ukimwi ni.....
viii. Unafikiri ni kwanini mwandishi amependekeza njia hiyo?
ix. Ni athari zipi zitakazolikumba Taifa endapo vijana wengi wataathirika na Ukimwi?
x. Nini maana ya msemo" usione soo"

2. Andika ufupisho wa habari hii usiozidi maneno 80.

SEHEMU B (ALAMA 25)

SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali yote katika sehemu hii:

3. Kwa kutumia mifano onesha matumizi ya viambishi vifuatavyo
   (a) "kwa" matumizi (03)
   (b) "Na" matumizi (01)
   (c) "Au' matumizi (01)
4. Toa fasili ya istilahi zifuatazo kama zitumikavyo katika lugha ya Kiswahili
   (a) Fonimu
   (b) Mofimu huru
   (c) Simo
   (d) Ngeli za nomino
   (e) Kishazi.
5. Kwa kawaida kamusi sanifu za lugha ya Kiswahili hupanga maneno yake kwa mpangilio maalumu wa kialfabeti, yapange maneno yafuatayo kwa kuzingatia mpangilio huo halafu eleza maana ya kila neno.
   a. Shajara
   b. Robota
   c. Nyukilia
   d. Oktoba
   e. Gwiji
   f. Plau
   g. Mkunde
   h. Haramu
   i. Imla
   j. Kingazija

6. Kimsingi mtumiaji wa lugha yoyote ile hubadilika kama kinyonga afanyavyo na rangi zake. Thibitisha kauli hii kwa mifano ya kutosha. Hoja tano.
7. Uchanganuzi wa sentensi hufuata hatua kwa hatua. Kwa kutumia hatua hizo changanua sentensi ifuavyo kwa njia ya jendwali.
"Mwalimu wa Kiswahili atawasili leo asubuhi".

SEHEMU C (Alama 10)

Jibu swali moja tu (1) katika sehemu hii

8. Andika kumbumbuku za kikao cha wanafunzi kuhusu hafla ya kumuaga makamu mkuu wa shule aliyepata wadhifa wa kuwa mkuu wa shule.
9. Andika mfano wa kadi ya mwaliko, huku ukizingatia mambo muhimu yanayopaswa kujumuishwa.

SEHEMU D (Alama 10)

MAENDELEO YA KISWAHILI

10. Kukuza na kueneza lugha sio kazi rahisi. Eleza juhudi zilizofanywa na mwingereza pekee ambazo hazikufanywa na taifa lingine katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini.

SEHEMU E (Alama 45)
FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali matatu (03) kutoka sehemu hii swali la 15 lazima.

11. Miongoni mwa kazi za msanii ni kuweka wazi maovu yaliyofichika na kuyakemea. Chagua waandishi wawili (2) wa Riwaya kati ya hao walioorodheshwa kisha eleza jinsi wanavyotekeleza wajibu wao.
12. Matumizi ya taswira na picha yanasaidia kuunda fasihi kisanaa na kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa, kwa mifano sita onesha ukweli huo ukitumia diwani mbili ulizosoma.
13. Mahusiano ya kimapenzi yanayofanywa ha vijana bila kufuata taratibu za ndoa, yana madhara makubwa katika jamii. Kwa kutumia vitabu viwili (2)vya tamthiliya kati ya hivyo vilivyotajwa, thibitisha ukweli huo huku ukioanisha na hali halisi ya jamii. Toa maoni yako kuhusu jinsi mwandishi alivyokabili mambo hayo.
14. Fasihi simulizi inahusu mambo ya kale ambayo yamepitwa na wakati yaani yamepitwa na usasa wa sayansi na teknolojia, hivyo hakuna haja ya kujifunza. Jadili kauli hii kwa kutoa mifano kuntu.
15. Wewe ni miongoni mwa watakao shiriki katika siku ya wanawake duniani itakayofanyika 2019. Andika ngonjera isiyopungua beti 05 isiyozidi beti 05 kuhusu " unyanyasaji wa kijinsia".

Tukiunganasisi sote

Hodi Hodi uwanjani,
Habarini kuwaletea,
Tujiunge sote
kupiga vita ukatili

Tegeni masikio
Habari

ORODHA YA VITABU

TAMTHILIYA

Orodha .....Steve Ranolds (MA)
Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe.....E. Semzaba (ESC)
Kilio Chetu.....Medical Aid Foundation (TPH)

RIWAYA

Takadini.....Ben Hanson (MBS)
Watoto wa Mama Ntilie.....E. Mbogo (H.P)
Joka la Mdimu.....A.J Safari (H.P)

USHAIRI

Wasakatonge..... M.S Khatibu (DUP)
Malenga Wapya.....TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka.....T.A Mvungi EP (D.LTD)

